

22- Al-Madd

المَدُّ Al-Madd:

Maana yake: Nyongeza kama Anavyosema Allaah (سبحانه وتعالى):

وَيُمَدُّكُمْ بِأَمْوَالٍ وَبَنِينَ ...

((Na Atakuongezeeni mali na wana ...))¹.

Katika hukmu ya Tajwiyd ni urefushaji au uongezaji wa sauti, kwa maana kuivuta sauti ya herufi wakati inapokutana na moja ya herufi za madd kuifanya iwe ndefu.

Herufi za madd ni tatu:

- ا Alif saakinah iliyotanguliwa na fat-hah: قَالَ
- ي Yaa saakinah iliyotanguliwa na kasrah: قِيلَ
- و Waaw saakinah iliyotanguliwa na dhwammah: يَقُولُ

Mifano katika maneno kutoka Aayah:

أُذِينَا	أُوتِينَا	نُوحِيهَا
Uuw dhiy naa	uuw tiy naa	nuw hiy haa

Madd imegawanyika sehemu mbili kuu:

- المَدُّ الطَّبِيعِي Al-Maddutw-Twabiy'iy pia huitwa: المَدُّ الْأَصْلِي - Al-Maddul-Aswliy
- المَدُّ الْفَرْعِي - Al-Maddul-Far-'iy

¹ Nuwh: (71: 12)